

MKATABA WA HUDUMA YA UTHAMINI

Mkataba huu umeandaliwa na kusainiwa na pande mbili leo tarehe.....ya Mwezi..... 2015, Bainya ya HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME wa S.L.P 138, SAME (Ambaye katika mkataba huu ataitwa (Mpokea Huduma) kwa upande mmoja.

NA

NDUNGU IRRIGATION SCHEME wa S.L.P.25, NDUNGU Ambaye katika mkataba huu ataitwa (Mtoa Huduma) kwa upande mwagine.

KWA KUWA Mtoa Huduma na Mpokea Huduma wakiwa na akili timamu na bila kushurutishwa na mtu ye yeyote wameamua kuingia mkataba kutoa huduma ya kuhost website kwa masharti yafuatayo:-

1. Mtoa Huduma amekubali kutoa huduma ya kuhost mtandao (website) wa Mpokea Huduma kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa malipo ya Fedha za Kitanzania shilingi laki tatu na elfu hamsini tu.(350,000/=).
2. Mpokea Huduma amekubali kumlipa Mtoa Huduma kiasi cha fedha tajwa katika mkataba huu ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuifanya iwe hai website ya mpokea huduma.
3. Mtoa Huduma amekubali kuwa atawajibika kulipa kodi ya huduma kwa Mpokea Huduma kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na itakatwa moja kwa moja kwenye malipo yake.
4. Mtoa Huduma amemhakikishia Mpokea Huduma kuwa atafanya kazi ya kuhost website ya Mpokea Huduma kwa weledi wa hali ya juu na kuhakikisha kuwa website hiyo inapatikana hewani kwa wakati wote..
5. Mpokea Huduma hatawajibika kulipia gharama zingine zitakazotokana na kazi ya kuhost website isipokuwa malipo yaliyokubalika kwa mujibu wa mkataba huu.
6. Mtoa Huduma amemhakikishia Mpokea Huduma kuwa atatumia wataalamu wenye taaluma inayotakiwa katika kuhost website ya Mpokea Huduma.
7. Mtoa Hudumu na Mpokea Huduma wamekubaliana kuwa mkataba huu ni wa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe za kuteuliwa.
8. Endapo itatokea upande wowote unataka kukatisha mkataba utatakiwa kutoa notisi ya maandishi ya mwezi mmoja kwa upande mwagine.

Mkataba huu utatafsiriwa chini ya Sheria za Mikataba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Endapo kutatokea kuvunjwa kwa masharti ya Mkataba huu hatua za kisheria zitafuatwa.

Kwa makubaliano hayo pande zote mbili zinatia saini zao hapa chini

kukubali kufungwa na masharti ya mkataba huu kama ifuatavyo:-

KWA NIABA YA MTOA HUDUMA KWA NIABA YA MPOKEA HUDUMA

JINA

JINA.....

SAINI.....

SAINI.....

CHEO.....

CHEO.....

TAREHE.....

TAREHE.....

SHAHIDI WA MTOA HUDUMA

SHAHIDI WA MPOKEA HUDUMA

JINA

JINA.....

SAINI.....

SAINI.....

CHEO.....

CHEO.....

TAREHE.....

TAREHE.....

Umeshuhudiwa na

JINA.....

SAINI.....

CHEO.....

TAREHE.....